**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

SOMO LA KWANZA KATIKA

# "Tuijuwe njiya ya wokovu"

## KWA KUJIFUNZA NA KUTII NENO LA MUNGU KWA KUTARAJIA UZIMA WA MILELE

**Utangulizi**

Mpendwa katika Kristo, ufuatao ni mfululizo wa masomo manane ambayo imeandaliwa kwa wakritso walio na nia ya kujuwa mambo ya muhimu kuhusu wokovu (kuufikiya na kuulinda) kwa nia ya kuepuka maangamizi ya milele inayotarajiwa kwa wale wasiojali neema kubwa Mungu alitupa kwa njiya ya Yesu Kristo.

Masomo haya yana mada zifuatazo:

Somo la 1: Maisha bila Kristo
Somo la 2: Wokovu kwa njiya ya Kristo
Somo la 3: Mamlaka ya Kristo
Somo la 4: Imani katika Kristo
Somo la 5: Toba kwa jina la Kristo
Somo la 6: Ubatizo katika Kristo
Somo la 7: Kanisa la Kristo
Somo la 8: Maisha mapya katika Kristo

"Na Filipo aliendа mahali alipo na kumsikia yule mtu anasoma kitabu cha nabii Isaya. Filipo akamwuliza, "Je, unaelewa maneno hayo unayoyasoma?" Yule towashi akasema, "Nitawezaje kuelewa pasipo mtu kunifafanulia?" Hivyo akamsihi Filipo ili apande na kuketi pamoja naye"

(Mdo. 8:30-31).

"Hivyo kwa mwaka mzima Barnaba na Sauli wakakutana na kanisa na kufundisha idadi kubwa ya watu. Ilikuwa ni katika kanisa la Antiokia kwa mara ya kwanza wanafunzi waliitwa 'WaKristo.'" (Mdo. 11:26).

"Lakini baadhi yao kwa ukaidi walipokataa kuamini na kukashifu ujumbe wake mbele ya umati wa watu, Paulo aliachana nao, akawachukua wanafunzi na kuhojiana nao kila siku katika darasa la mtu mmoja aitwaye Tirano" (Mdo 19:9).

"Watu hawa walikuwa wema kuliko wale wa Tesalonika, wa sababu walipokea Neno kwa nia iliyokuwa tayari kabisa, wakatafuta Maandiko kila siku kujuwa hakika ya maneno yale (waliofunzwa)"
(Mdo. 17:11).

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

Mungu akubariki na kukuumbiya imani safi, juhudi na moyo wa utiifu kwa haya unayoyasoma.

# Somo la kwanza: Maisha bila Kristo

Injili (maana halisi: Habari Njema) ya Kristo, ambayo ndiyo mada ya jumla ya mfululizo huu wa mafundisho, ipo ya maana kwa sababu mwanadamu ana haja ya wokovu kwa njia ya Yesu Kristo. Haja hii ni kutokana na uwezo wa laana wa dhambi, na maangamizi yake pia matokeo yake mabaya katika maisha ya kila mtu. Lakini kabla ya binadamu yeyote anayeishi bila Kristo awe na nia ya kutafuta baraka za ajabu kwake zinazopatikana katika injili ya Kristo, ni lazima aamini kuwa yeye ni mwenye dhambi na kwamba bila msaada wa neema ya Mungu, kinachomungoja ni kuishi bila tumaini lolote katika ulimwengu wa sasa na kuangamia milele katika ulimwengu ujao.

Katika kitabu cha Matendo ya Mitume, sura ya 2, aya yake ya 14 hadi 40; tunapata ushahidi wa mahubiri ya kwanza ya Injili. Katika hotuba hii, mtume Petro alisema bila shaka kwa wasikilizaji wake, kwamba walikuwa wenye dhambi na walikuwa hasa na hatia ya uhalifu kuona kwamba walimsulubisha Yesu Kristo mwana wa Mungu aliye hai (mstari wa 36). Aya ifuatayo inasema: "*Baada ya kusikia hayo, waliguswa mioyoni mwao na wakamwambia Petro na mitume, Ndugu zangu, tufanye nini?*" Kwa nini watu waliwauliza mitume la kufanya ili kupata wokovu wa Bwana? Kwa sababu walisadiki kuwepo kwa dhambi ndani mwao na hasara yake kubwa isipokuwa wawe wameokolewa kutoka hayo. Vile vile, watu wa siku za leo wangeuliza wazi: "Tufanye nini?" na wangetafuta msaada wa Bwana, punde tu wanapotambua kwamba wao ni wenye dhambi zinazowapeleka kwenye maangamizi ya milele.

Sasa tuchunguze kwa makini na bila upendeleo, mafundisho ya msingi wa Neno la Mungu kuhusu dhambi.

1. **Ufafanuzi wa dhambi:** "*Kila mtu atendaye dhambi ameasi (ni muasi) na dhambi ni uasi wa sheria* (1 Yohana 3:4). Maelezo ambayo kifungu hiki kinatupa kuhusu dhambi ni kwamba, chochote katika maisha ya mtu ambacho kipo kinyume na haki iliyofunuliwa katika Neno la Mungu, katika Injili ya Yesu Kristo (Agano Jipya). Soma pia 1 Yohana 5:17. Mtu huasi, sio tu kwa kutenda maovu waziwazi, bali pia kwa kushindwa kutenda mema (Yakobo 4:17). Zaidi tena, Agano Jipya hufundisha kwamba si matendo ya nje tu inayothibitisha dhambi, bali pia nia, zamiri na tamaa mbaya (Mathayo 5:21, 22, 27, 28; Marko 7:21; 1 Yohana 3:15). Soma kwa makini katika maandiko yafuatayo ya Agano Jipya, ambayo pamoja na mengine, yanahakikisha kuwepo kwa dhambi zichukizazo Mungu na kuharibu sifa njema ya kila azitendaye. Dhambi hizo ni kama uasherati, uzinzi, ulevi, uongo, wizi, uuaji, wivu, chuki, tama mbaya, waabudu

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

sanamu, nk. Mathayo 3:19; 1 Wakorintho 6:9-10, Wagalatia 5:19-21; Waefeso 4:25-31; 5:3-5; 2 Timotheo 3:2-4; 1 Johana 3:15.

**2. Dhambi zimewakumba wote ulimwenguni.** Dhambi imepata moyo wa kila nafsi imewahi kuishi, isipokuwa tu Mwana wa Mungu aliyekuwa bila hatia. Hakuna anayeweza kusema kwamba hana hatia mbele ya mahakama ya Mungu. "*Kwa sababu sisi tayari tumekwisha onesha wazi kwamba Wayahudi, Wayunani, ni chini ya utawala wa dhambi, kama ilivyoandikwa: Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja ... kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu*" (Warumi 3:9-10, 23). Pia soma 1 Wafalme 8:46, Isaya 53:6, Zaburi 130:3, Wagalatia 3:22. Wale ambao hutaka kujihesabiliya wenyewe haki kutokana tu na maadili yao mema au tena kwa matendo mema wanayoyafanya binafsi machoni pa watu, wanajidanganya sana. Dhambi yao iwe kubwa au ndogo, nyingi au chache, wote wana hatia ya kuvunja sheria za Mungu; kwa hiyo ni lazima kutambua kwamba wao ni wenye dhambi na hukumu ya Mungu inawangoja, kabla ya kufikia neema na kuomba huruma ya Mungu. Kumbuka kuwa mtu mzima yeyote lazima akubali kwamba ana hatia mbele za Mungu, kufuatana na jinsi dhambi, bila kuwa na upendeleo pia heshima na mtu yeyote, imewapata watu wote tangu viongozi hadi watu wa ngazi ya chini (Hesabu 20:12) na hata yule anayeonekana myenyekevu kuliko wote. Imepata vilevile msaliti mlafi na mwanafunzi yeyote yule angelifikiriya yuko salama (Yohana 18:1-5 inayotowa mfano wa Yuda; Yohana 18:15-27 inayotowa mfano wa Petro).

**3. Asili ya dhambi.** Mwanzilishi wa dhambi ni bila shaka Ibilisi au Shetani, : "*Ni yeye aliyetenda dhambi tangu mwanzo*" (1 Yohana 3:8). Soma Mathayo 13:38-39; Jean 8:41-44, 1Yohana 3:10. Njia inayotumiwa na Shetani kuwavuta wanadamu katika dhambi ni kuwashawishi kwa ndani na kwa nje (Yohana 13:02, Matendo 5:3, 1 Wakorintho 7:5, 1 Wathesalonike 3:5). Vishawishi ni huko kufuata tegemeo la mwili, shaui la akili na tamaa za mwili (1 Yohana 2:16; Yakobo 1:14). Lakini, lazima tukumbushe kwamba sio kila kujaribiwa (kushawishika) ndiko kunafuatana na dhambi. Kuna kujaribiwa na kusimama imara bila kutenda dhambi. Soma Yakobo 1:12. Bwana wetu "*alijaribiwa kama sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi*" (Waebrania 4: 15). Soma Mathayo 4 :1-11. Basi, mtu hutenda dhambi wakati ule jaribu (au kishawishi) linamfikisha kwenye dhambi (Yakobo 1: 14,15), na hivyo kutoa nafsi yake kwa shetani. Adam na Hawa, amba ndio binadamu wa kwanza kufanya dhambi, hawakuitenda sababu tu ya kujaribiwa na Shatani bali hapo tu walipoamini na kutii shauri la mshawishi pia maagizo yake, hapohapo wakaasi sheria ya Mungu (Mwanzo 3 :1-7). Vivyo hivyo leo, wakati watu hutii na kufuata shauri la Shetani, wao huwa waasi wa sheria ya Mungu (Neno lake) na hapohapo wana hatia dhidi ya dhambi. Wengine hudai kwa udanganyifu kwamba Mungu atawavumilia

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

katika uzaifu wao na kuwaonea huruma. Tukumbuke kwamba malaika walioasi hakuwahurumiya.

**4. Madhara na matokeo ya dhambi.** Hakuna anayeweza kuzarau shauri la kuacha dhambi wakati tunapoangalia madhara ya kutisha na matokeo yake tangu zamani hadi leo, hata kesho. Kwa kutaja mifano ya madhara na uharibifu wa dhambi kwa binadamu, tunaweza taja tu: nyumba ambazo zimevunjika, vifungo vya gerezani, maisha ya laana na ya kuchanganyikiwa, uporaji, uhalifu wa kila aina, vita vya mauwaji ya kikabila, kutegemea viumbe kuliko Muumba, … na mengineo zaidi ya maelfu ya matokeo mabaya katika ulimwengu huu.

Basi tujaribu kuona, kwa mwangaza wa Neno la Mungu, matokeo mabaya na ya kusikitisha ya mwenye dhambi katika maisha haya. Amekuwa bila Kristo na bila Mungu (Waefeso 2:12). Ametengwa na Mungu (Isaya 59:2). Yeye anaishi katika giza (Wakolosai 1:13, 1 Petro 2: 9, 1 Yohana 2: 11). Ni mtoto wa shetani (Yohana 8:44). Kiroho ni mgonjwa (Mathayo 9:12). Yeye ni mtumwa wa dhambi (Warumi 6:16). Yeye ni mpotevu (Luka 19:10). Ana mzigo wa maovu (Mathayo 11:28) nk. Matokeo ya kutisha sana ya dhambi ni kifo cha roho. Katika hali halisi, kuna vifo vya aina mbili katika Biblia: kwanza ni kifo cha mwili, pia kifo cha roho.

Hiki kifo cha mwili ni matokeo ya dhambi ya Adamu bali si matokeo ya dhambi zetu binafsi. Watu wote, bila kujali hali yao ya kiroho, wanapatwa na matokeo ya dhambi ya Adam, yaani kifo cha asili, cha mwili. Aidha, ufungulifu kutoka kifo hiki hauna uhusiano wowote na hali ya kiroho ya watu, kwa sababu kwa njiya ya ufufuo wa Kristo, na watu wote (waliokufa katika dhambi na waliokufa wakiwa waaminifu kwa Mungu), watafufuka kutoka wafu. “Maana *kama vile kifo kilikuja kwa njia ya mtu mmoja (Adam), pia kwa mtu mumoja (Kristo) ukaja ufufuo wa wafu. Na kama katika Adamu wote wanakufa, hivyo wote pia watafufuliwa kwa njiya ya Kristo*” (1 Wakorintho 15:20-21). “*Msishangae kusikia haya, kwa maana saa inakuja ambapo wale walio makaburini wataisikia sauti Yake. Nao watatoka nje, wale waliotenda mema watafufuka wapate uzima na wale waliotenda maovu, watafufuka wahukumiwe*.” (Yohana 5:28,29).

Biblia haifundishi kwamba watu watahukumiwa kwa ajili ya dhambi ya Adamu. Lakini tu kwa ajili ya dhambi zao wenyewe (Warumi 14:12; 2 Wakorintho 5: 10). Ni kweli kwamba asili ya kufanya dhambi imeambukiya ulimwengu kutoka kwa Adam, hata vizazi na vizazi, kupitiya hali yetu ya mwili wa binadamu ; hata hivyo, Mungu hatuhukumu kwa sababu ya hii hali yetu bali tu kwa ajili ya kukosa kutimiza mapenzi yake (ambayo ni wazi katika Neno lake) na hiyo ndiyo inawajibika kwa kila mtu binafsi.

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

Adhabu ya dhambi zetu binafsi ni hiyo mauti ya pili, kufa kiroho: "*Lakini waoga, wasioamini, wachafu, wauaji, wazinzi, wachawi, waabudu sanamu, pamoja na waongo wote, mahali pao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili".* (Ufunuo wa Yohana 21:8). "*Mshahara wa dhambi ni mauti*" (Warumi 6:23). Angalia Yakobo 1:15. Maana ya kifo kuhusiana na ziwa la moto katika Jehanamu ni kutengwa milele kutoka kwa Mungu na kwa Kristo, kutengwa na pahali pa utukufu wa Mungu yaani mbinguni. Yesu akawaambia wale ambao waling'angania dhambi zao: "*Mimi naenda, nanyi mtanitafuta, na mtakufa katika dhambi zenu ; ninyi hamwezi kufika ninakokwenda*" (Yohana 8: 21). Soma 2 Wathesalonike 1:7-9.
Hakika Jehanamu iko, siyo tu mahali watu hufikiri kwa kuwaogopesha wengine, au tena kivuli kitupu; la hasha. Wale watakaokufa katika dhambi watachukuwa, watapatwa na maumivu pia uchungu wa kutisha ulio pahali hapo. "*Kutakuwa na kilio na kusaga meno*" (Mathayo 13:42). "*Na watateswa mchana na usiku, milele na milele*" (Ufunuo wa Yohana 20:10). Soma Mathayo 25:46, Marko 9:43-48, Luka 13:25-28, 1 Wakorintho 6:9, Wagalatia 5:21, Waefeso 5:5, Waebrania 10:27-31 ; Ufunuo wa Yohana 21:27, 22: 14-15.

Jehanamu haikuandaliwa kwa ajili ya watu, bali kwa ajili ya shetani na malaika wake. Lakini, baada ya watu kuchagua kumfuata shetani, wakiwa na uzowefu wa kufanya dhambi katika maisha yao yote, nao huchagua wakati huohuo njiya na hasara ya mwisho ya Shetani. Hakika, si mapenzi ya Mungu kwamba watu wapoteye na kuangamiya. Kinyume na wazo hili, Biblia inatufundisha kwamba Mungu aliupenda sana ulimwengu : "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele*" (Yohana 3:16). Kristo atawaambia waovu, "*Ondoka kwangu, mliolaaniwa, nendeni katika moto wa milele, ambao uliandaliwa kwa ajili ya Shetani na malaika wake*" (Mathayo 25:41). Ikiwa mapenzi ya Mungu ilikuwa kuona watu wakiangamiya, basi tunaweza sema kwamba Jehanamu kama adhabu juu ya dhambi, sio haki kabisa. Lakini hii si mapenzi ya Mungu kwamba watu wapoteye (2 Petro 3:9). Aidha, tungelifikiri zaidi na kusema kwamba jehanamu ni adhabu isiyo haki dhidi ya dhambi ikiwa hakungelikuwa njiya ya kuokolewa. Lakini Mungu, kwa huruma wake mwingi, amewapa watu wote nafasi ya kuepuka hatia na uwezo wa dhambi, kama vile tutaona katika somo lifuatalo kisha tu hili la kwanza. Hata hivyo, watu wako huru, wakiwa na haki ya kuchagua njia inayoongoza kwenye uzima au ile ipelekayo mautini. Maoni yetu sio kuona watu wanachaguwa njiya ya mauti bali ile ya uzima, kama ilivyo mapenzi ya Mungu. Tunajuwa basi kwamba, Mungu hatashurtisha mtu kuacha njiya ya mauti na kuja kwake ila uamzi wa hiari wa kila mumoja anayetambuwa hatari na matokeo mabaya ya maisha katika dhambi. Soma Yohana 5:40; Ufunuo 22:17.

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

***Je, wewe bado ungali katika dhambi?***
***Unaishi bila Kristo?***
***Umehisi kwamba muda wako haujafika?***
***Umejaribu kuokoka bali shetani kakurudisha nyuma?***

Ikiwa majibu ni ndiyo, hujaona madhara na matokeo mabaya ya maisha katika dhambi, wala wewe hujaelewa ni kiasi gani unahitaji msaada wa Mungu? Umepata faida gani katika maisha bila Kristo, ya kuchanganyikiwa na ya unafiki katika madhehebu? Hakuna hata faida moja kwa kuwa kuna wale wangedanganyika kujifariji eti hata wakiwa katika dhambi wana mali ya dunia, Biblia inasema kwamba ni upepo, ni ubatili, ni bure hata ingekuwa ni dunia yote (Mathayo 16:26). Kumbuka mfano wa tajiri na maskini Lazaro (Luka 16:25).

Katika somo litakalofuata (la pili), tutapata kujuwa na kueleza wazi kuhusu njia ambayo Mungu ameweka kwa kuepuka dhambi na maangamizi yake ya kutisha kwa mwangaza wa Injili ya Yesu Kristo.

✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧☆☆☆☆☆☆☆☆☆✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧

Ikiwa una maswali yoyote wala kutaka mwangaza wa zaidi,

✍Andikiya:

- Kanisa la kristo pa Bukavu, SLP/Po Box: 222, Cyangugu-Rwanda.
- Email: klk.bukavu@yahoo.fr

⇨ Kutana na watumishi wa Mungu pahali wanaposhiriki pamoja na kanisa kwenye anuani ifuatayo:
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – DRC.